

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



29 JANUARI, 2015



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA NANE

KIKAO CHA TATU – TAREHE 29 JANUARI, 2015

I. **MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

II. **MASWALI YA KAWAIDA:**

OFISI YA WAZIRI MKUU:

30. MHESHIMIWA PROF. PETER MAHAMUDU MSOLLA (KILOLO):


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Mji mdogo wa Ilula umeanza kupata adha kubwa ya utoaji maji taka:-

Je, ni lini sasa mji huo ulio Wilayani Kilolo utapewa huduma ya kutoa maji taka.

OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):

31. MHESHIMIWA MARYAM SALUM MSABAHA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora):- Kumekuwa na baadhi ya Viongozi wa Serikali waliojilimbikizia mali kwa njia ambazo si halali:-

- 
- (a) Je, ni Viongozi wangapi ambao mali zao wanazipata kwa njia hiyo au kwa rushwa zimetaifishwa;
 - (b) Je, Serikali imechukua hatua gani za kisheria kwa baadhi ya Viongozi wenye mishahara ya kawaida lakini pia wanamiliki mali zenyenye thamani kubwa.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:

32. MHESHIMIWA MARIAM REUBEN KASEMBE (MASASI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto:- Madhumuni ya kuanzisha Benki ya Wanawake ilikuwa ni kuwawezesha Wanawake kujikomboa kiuchumi:-

- (a) Je, ni Wanawake wangapi wamenufaika na Benki hiyo, na ni kutoka Mkoa gani;
- (b) Je, ni vikao vingapi vyatyanahisa vimefanyika tangu mwaka 2007 ilipoanzishwa Benki hiyo.

WIZARA YA FEDHA:

33. MHESHIMIWA DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALLA (NZEGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, kwa nini Serikali inakusanya kodi kwa wananchi na kisha inawachaji huduma za afya, elimu na maji badala ya kutoa huduma hizo bure.




WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

34. MHESHIMIWA AHMED MABKHUT SHABIBY (GAIRO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Serikali ina nia nzuri ya kuwasambazia Wananchi umeme kupitia mradi wa REA ambao awamu ya pili inakamilika mwezi Juni, 2015; hata hivyo, katika baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Gairo REA bado hawajasaini mkataba na Mkandarasi wa kusambaza umeme vijijini:-

- (a) Je, kwa nini REA wasimsainishe Mkandarasi huyo ili kazi hiyo ianze mara moja;
- (b) Je, Serikali inatoa uthibitisho gani kuwa vijiji vyote vilivyopitishwa katika Bajeti ya mwaka 2014/2015 vitapatiwa umeme kabla ya muda huo kuisha;
- (c) Je, Serikali haionti kuwa inashindwa kutekeleza ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais ya kuwapatia umeme Wananchi wa vijiji vya Wilaya ya Gairo.



WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

35. MHESHIMIWA LETICIA MAGENI NYERERE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Asilimia ishirini (20%) ya Wanawake wa Mkoa wa Mwanza hawana elimu ikilinganishwa na Mikoa mingine kama Kilimanjaro (2.8%) na Dar es Salaam (6.9%):-

- (a) Je, Serikali inatoa ufanuzi gani kuhusu tofauti hiyo;

- (b) Je, Serikali inashauri nini kifanyike ili kupunguza idadi ya Wanawake wasio na elimu Mkoani Mwanza.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

36. MHESHIMIWA HERBERT JAMES MNTANGI (MUHEZA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Wananchi wa Wilaya ya Muheza wanamshukuru sana Mhe. Rais kwa kufuta hati za mashamba ya Mkonge ya kwa Fungo, Bwembera, Kihuhwi, Segalasi, Lewa, Azimio/Kilapula:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kuisaidia Wilaya ya Muheza gharama za upimaji wa haraka wa mashamba hayo ili kuwagawia Wananchi wenyewe shida ya ardhi;

(b) Je, Serikali inatambua kwamba kuchelewa kupima na kugawa mashamba hayo kutasababisha uvamizi mkubwa na hatimaye mapigano na mauaji ya Wananchi.

WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:

37. MHESHIMIWA MUHAMMAD IBRAHIM SANYA (MJI MKONGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:- Njia ya kuwahabarisha raia wa nchi yoyote Duniani ni kuitia Redio, Televisheni na Magazeti, njia ambazo ni ghali mno ikilinganishwa na hali halisi ya kipato cha wananchi vijijini, na ili kuhakikisha kuwa raia walio wengi wanapata habari kwa muda muafaka Serikali inatakiwa iwe na mikakati maalumu ya kupunguza ghamama za upatikanaji wa vyombo hivyo vya habari:-

Je, ni lini Magazeti yatapunguzwa bei ili watu wengi zaidi waweze kununua na kupata taarifa za matukio mbalimbali yanayotokea nchini na kuelimika pia kwa taarifa mbalimbali zikiwemo za kisiasa na kiuchumi.

**III. HOJA YA KUJADILI JAMBO LA DHARURA
LILILOTOKEA:**

MHE. JAMES FRANCIS MBATIA, (MB)

IV. KAULI ZA MAWAZIRI:

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

V. HOJA ZA KAMATI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:



Kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali pamoja na mapendelekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Bajeti pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

DODOMA
29 JANUARI, 2015

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE